Research Journal in African Languages

RJAL



Research Article

Section: Literature, Linguistics & Criticism

Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global.

Volume 5, Issue 1, 2024

**Article Information**
Submitted: 6th February 2024
Accepted: 30th March 2024
Published:14th April 2024

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

To read the paper online, please scan this QR code

# Morphological patterns of Kamba place names: A lexical morphology perspective

**Peninah Mwende Musyoki, Vifu Makoti, John Mutua**
Department of Linguistics and Languages, Machakos University, Kenya
Correspondence: peninahmwendem@gmail.com

**Abstract**
This article has investigated the morphological patterns of Kamba place names by examining the various components which form those names. The names herein examined are part of a larger data collected from Makueni sub-county. Place names and their units have been presented using tables and tree diagrams. The results of this investigation have shown that a large percentage of names in the Kamba community have various components which join up to make them. The components have been morphologically analysed. This conclusion contradicts the claims structuralists like Agard (1984) that specific names like place names are formed only by roots. This article has proven that there exist special components that make up toponyms.

**Keywords:** lexis, morphology, onamastics, place names, toponyms

**How to Cite:**
Ruwaza za kimofolojia za majina ya mahali ya Kikamba: Mtazamo wa mofolojia leksia. (2024). *Research Journal in African Languages*, *5*(1). https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/1553

© 2024 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

Research Article

Section: Literature, Linguistics & Criticism

Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global.

Volume 5, Issue 1, 2024

**Article Information**
Submitted: 6th February 2024
Accepted: 30th March 2024
Published:14th April 2024

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

To read the paper online, please scan this QR code

# Ruwaza za kimofolojia za majina ya mahali ya Kikamba: Mtazamo wa mofolojia leksia

**Peninah Mwende Musyoki, Vifu Makoti, John Mutua**
Department of Linguistics and Languages, Machakos University, Kenya
Correspondence: peninahmwendem@gmail.com

**Ikisiri**
Makala hii imechunguza ruwaza za majina ya mahali ya Kikamba kwa kuangalia vijenzi mbalimbali vinavyojenga majina hayo. Majina yaliyoshughulikiwa ni sehemu ya data iliyokusanywa kutoka Jimbo dogo la Makueni. Majina ya mahali na vijenzi vyake yamewasilishwa kwa kutumia majedwali na michoro msonge. Matokeo ya uchanganuzi huo yamedhihirisha kuwa asilimia kubwa ya majina ya mahali katika jamii ya Wakamba yameundwa kwa vijenzi mbalimbali ambavyo huungana kuyaunda. Vigezo hivyo vimechanganuliwa kimofolojia. Ukweli huu unapinga madai ya wanamuundo kama Agard (1984) kwamba majina ya mahusus kama ya mahali huundwa kwa mizizi tu, Makala hii imethibitisha kuwa vipo vipashio maalumu vinavyounda majina ya mahali.

**Istilahi muhimu:** leksia, majina ya mahali, mofolojia, ruwaza, vigezo

**How to Cite:**
Ruwaza za kimofolojia za majina ya mahali ya Kikamba: Mtazamo wa mofolojia leksia. (2024). *Research Journal in African Languages*, *5*(1). https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/1553

© 2024 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

## 1.0 UTANGULIZI

Majina ya mahali yamekuwa yakitazamwa kama maneno yaliyoundwa kwa mofimu moja tu hata katika lugha ambishi-bainishi kama za Kibantu. Wanaisimu kama Agard, (1984) na Habwe na Karanja (2007) walitoa madai kwamba nomino mahususi huundwa na mzizi tu, hivyo haziwezi kuchanganuliwa kimofolojia. aHHHhhab Hali hii huenda ndiyo imesababisha uhaba wa tafiti katika tawi hili la lugha. Watafiti kama Kadmon, (2000), Karama, (2022) na wengine wameshughulikia majina ya mahali kisemantiki. Wengine kama Beberwa, (2011), Choge, (1997), Kirui, (2013), Anido, (2016) na wengine wamegusia baadhi ya vipengele vya kimofolojia vya majina ya mahali. Makala hii imeangazia vijenzi mbalimbali vya majina ya mahali ya Kikamba kwa lengo la kubainisha vijenzi maalumu vya majina katika lugha hiyo. Uchunguzi huu ni wa kimofolojia.

## 2.0 Makundi ya Nomino katika lugha ya Kikamba (Cha Machakos na Makueni)

Kwa kuwa lengo la makala hii ni kubainisha vijenzi mbalimbali vinavyounda majina ya mahali ya Kikamba, ni vizuri kudokeza kuhusu makundi ya nomino za lugha ya Kikamba kwa kutegemea upatanisho wa kisarufi katika lugha hiyo. Kwa mujibu wa mtafiti majina ya Kikamba yamegawika katika makundi kumi (10) yafuatayo.

**Jedwali 2.1 Ngeli za Nomino Katika Lugha ya Kikamba**

| Nambari | Viambishi vya Kundi/ Ngeli | Mifano ya Nomino | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | WA-MA | mundu – andu | mtu -watu |
| 2. | WA-YA | muunda -miunda | shamba- mashamba |
| 3. | KYA-SYA | kivila – ivila | kiti – viti |
| 4. | YA -MA | yiembe – maembe | embe – maembe |
| 5. | WA -SYA | usi – mbusi | mto –mito |
| 6. | YA -SYA | Nyumba -nyumba | Nyumba-nyumba |
| 7. | MA-MA | Mauta -mauta | Mafuta -mafuta |
| 8. | WA -WA | muthanga - muthanga | Mchanga -mchanga |
| 9. | KYA -KYA | Kiw'u - kiw'u | Maji -maji |
| 10. | VANDU – VA<br><br>VANDU -KU | | MAHALI -PA<br><br>MAHALI -KU |

Asili: Peninah Musyoki (2024)

Katika Makala hii imebainika kwamba baadhi ya viambishi katika majina ya mahali ya Kikamba vinawakilisha ngeli za majina hayo. Kwa mujibu wa Buberwa (2011), viambishi hivi huambatanishwa na nomino za kawaida ili kuunda majina ya mahali.

## 3.0 Uchanganuzi wa Vijenzi Mbalimbali Vinavyounda Majina Mahali ya Kikamba

Kisintaksia majina ya mahali katika lugha ya Kikamba yanaweza kugawika katika makundi mawili makuu; majina yenye muundo wa neno moja tu na majina yenye muundo wa maneno mawili au zaidi, Makala hii imeshughulikia majina ya mahali yaliyoundwa kwa neno moja tu. Makala hii imebaini kwamba mengi ya majina ya mahali ya Kikamba yaliyoundwa kwa neno moja yamejidhihirisha kama nomino ambazo asili yake ni nomino nyingine. Majina haya yamejengwa kwa mofimu mbalimbali ambazo zinaungana kuunda jina moja kama ifuatavyo;

### 3.1 Muundo wa Mzizi na Kiambishi Kielezi cha Mahali -ni (mz+E-ni)

Majina katika kategoria hii yana mofimu mbili tu. Mofimu ya kwanza ni mzizi wa kitenzi na ya pili ni kielezi cha mahali (-ni). Mifano ifuatayo inadhihirisha haya.

**Jedwali 3.1.1: Mifano ya Majina ya Mahali yenye Muundo wa (mz +E)**

| Nambari | Majina | Vijenzi vyake | Tafsiri ya lKiswahili |
|---|---|---|---|
| 1, | *Nthongo* | Nthongo-ni | Mahali penye chemichemi ya maji |
| 2. | *Nthangathini* | Nthangathi-ni | Mahali penye changarawe |
| 3. | *Munyuni* | Munyu-ni | Mahali penye chumvi |
| 4. | *Mbokani* | Mboka-ni | Mahali pa mboga |

Majina yaliyo katika kategoria hii yamejengwa kwa mzizi na kiambishi tamati **-ni** kinachoonyesha mahali katika lugha ya Kikamba.

**Kielelezo 1:** ***Mchoro wa Msonge Unaoonyesha Majina ya Mahali Yaliyojengwa kwa (mz+E-ni)***

### 3.2 Muundo wa Viambishi Ngeli, Mzizi na Kielezi -ni cha Mahali (ng+Mz +E-ni)

Majina ya mahali  ya Kikamba katika kategiria hii yameundwa na kiambishi cha ngeli na mzizi kama inavyodhihirika katika jedwali (3.2.1) lifuatalo: Kimsingi nomino zinapoambishwa -ni mwishoni hubadilika na kuwa vielezi lakini katika muktadha huu wa majina ya mahali, maneno hayo yametumiwa kutaja mahali mbalimbali kama ifuatavyo:

**Jedwali 3.2.1: Mifano ya Majina ya Mahali yenye Muundo wa (ng+mz+E-ni)**

| Nambari | Jina | Vijenzi vyake | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | *Mithumoni* | mi-thumo-ni<br>ng2+mz+E | Sehemu ya nyuma ya mguu yenye nyama nyingi ikilinganishwa na zingine zizivo chini ya goti. |
| 2. | *Mutauni* | Mu-tau-ni<br>Ng2+mz+E | Mtaroni |
| 3. | *Kithoni* | Ki-tho-ni<br>Ng3 +mz+E | Sehemi yenye chemichemi ya maji |
| 4. | Iviani | I-via-ni<br>Ng4+mz+E | Jiweni |

Mifano katika jedwali (3.2.1) inaonyesha kuwa majina ya mahai ya Kikamba hujengwa kwa viambishi ngeli tofauti tofauti. Kwa mfano, jina *Mithumo* ambayo iko katika hali ya wingi ina kiambishi kya ngeli **mi-** ambacho ni wingi wa **mu** katika nomino *Muthumo*. Nomino hii iko katika ngeli ya WA-YA. Katika mfano wa pili, jina *Mutauni* ni umoja wa *Mitauni*. Nomino hiyo iko katika ngeli iyo hiyo ya WA-YA pia. Kiambishi cha ngeli katika jina *Mitau* ni **Mi-** Mfano wa tatu unataja nomino katika ngeli ya KYA-SYA. Neno *Kitho* ambalo liko katika hali ya umoja lina kiambishi cha ngeli **Ki-** wingi wake ni *Syitho*. Mfano wa mwisho katika kategoria hii  unataja nomino katika hali ya umoja. Neno *Iviani* lina Kiambishi **I-** cha ngeli ya **YA-MA.** Wingi wa nomino *ivia* ni *Mavia*. Majina yote kikundi hiki yana

kiambishi tamati **-ni** baada ya mzizi. Katika lugha ya Kikamba kiambishi hiki huashiria mahali.

**Kielelezo 2: Mchoro Msonge Unaoonyesha Mfano wa Majina ya Kikamba Yaliyojengwa kwa (ng+ mz+ E)**

**3.3 Muundo wa Kiambishi Kikanushi cha Nafsi, Mzizi na Kiishio -a (k/nafsi+mz+kiishio)**

Katika sampuli aliyotumia mtafiti kulikuwa ma jina moja la mahali lililoundwa kwa Kiambishi kikanushi cha nafsi ya pili (umoja) na mzizi wa neno kama ifuatavyo:

**Jedwali 3.3.1: Mfano wa Jina Lililojengwa kwa (K/na+mz+kiishio)**

| Nambari | Majina | Vijenzi vyake | Tafssiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | *Ndukuma* | Ndu-kum-a | Hutoki |

Jina hili limeundwa kwa kiambishi kikanushi cha nafsi ya pili umoja **ndu**- na mzizi. Jina hili katika hali ya wingi lingekuwa *Muikuma*. Viambishi vinavyoashiria ukanusho ya nafsi ya pili wingi ni **mui-**

**Kielelezo 3: Mchoro wa Msonge Unaoonyesha Jina Lililojengwa kwa (k/nafsi+mz +kiishio)**

**3.4 Muundo wa Kiambisi cha Udogo, Mzizi na Kiambishi Kielezi cha Mahali (K/udg+mz+E)**

Kiambishi kinachoashiria udogo au dharau katika lugha ya Kikamba ni **ka**-. Majina ya mahali katika kategoria hii hujengwa kwa kiambishi hicho pamoja na mzizi au shina la neno. Majina haya yanaweza kuwa ya miti, milima au wanyama kama inavyodhihirika katika jedwali linalofuata;

**Jedwali 3.4.1: Mifano ya Majina ya Mahali Yaliyoundwa kwa (K/udg+mz+E)**

| Nambari | Majina | Vijenzi vyake | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | *Kamunyee* | Ka-munyee | Kijito chembamba |
| 2. | *Kaseve* | Ka-seve | Upepo mdogo mwanana |
| 3. | *Kavingo* | Ka-vingo | Mpingo mdogo |
| 4. | *Kangondi* | Ka-ngondi | Mlima mdogo ambapo ngati walipatikana |
| 5. | *Kayumba* | Ka-yumba | Mahali padogo penye matope |

Majina yote katika kundi hili la majina yana kiambishi cha udogo **ka-** kikiambatanishwa na shina la neno.

**Kielelezo 4: Mchoro wa msonge unaoonyesha majina ya mahali yanayojengwa kwa (K/udg+mz+E)**

**3.5 Muundo wa Kiambishi cha Udogo, Mzizi na Kiambishi cha Mahali -ni (k/udg+mz+E)**

Majina ya mahali yaliyo katika kikundi hiki yana kiambishi **ka-** kinachoonyesha udogo katika lugha ya Kikamba, **mzizi** wa neno na kiambishi tamati **ni-** cha mahali. Muunndo huu unadhihirika katika jedwali linalofuata.

**Jedwali 3.5.1: Mifano ya Majina ya Mahali Yaliyoundwa kwa (k/udg+mz+E)**

| Nambari | Majina | Vijenzi vyake | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | *Kaumoni* | Ka-umo-ni | Mahali palipo na mgumo mdogo |
| 2. | *Katoloni* | Ka-tolo-ni | Mahali palipo na mti mdogo wa *kitoo* |
| 3. | *Kavisuni* | Ka-visu-ni | Mahali panapohusishwa na chungu kidogo |
| 4. | *Kaiani* | Ka-ia-ni | Mahali pa ziwa dogo |

Jina *Kaumoni* linatokana na jina *Kiiumo* ambalo linarejelea mti unaoitwa mgumo. Kiambishi **ka-** kinaleta dhana ya udogo wa nomino inayorejelewa. *Kavingo* ni udogo wa *Kivingo* ambalo ni jina la mti unaoitwa mpingo katika lugha ya Kiswahili. Kiambishi **ka-** kinaonyesha udogo. *Kavisu* ni chungu kidogo kwa hivyo jina hilo likiongezwa kiambishi **ni**-mwishoni kinaleta dhana ya mahali palipo na chungu kidogo au panapohusishwa na utengenezaji wa vyungu vidogo. Katika lugha ya Kikamba, *Kaia* ni udogo wa *yiia* ambayo humaanisha ziwa dogo. Kiambishi tamati **ni-** mwishoni wa nomino hiyo kinaleta dhana ya mahali.

**Kielelzo 5: Mchoro wa Msonge Unaoonyesha Majina ya Mahali Yaliyojengwa kwa (K/ udg+mz na E)**

### 3.6 Muundo wa kiambishi cha wingi na mzizi (K/wi+mz)

Majina katika kategoria hii yameundwa kwa mofimu mbili; ya kwanza ni kiambishi cha wingi wa nomino na ya pili ni mzizi wa neno linalorejelewa. Mofimu hizi zimewekwa pamoja kuunda jina la mahali. Mifano ya majina iliyo katika jedwali linalofuata inadhihiriha hali hii.

**Jedwali 3.6.1: Mifano ya Majina ya Mahali Yenye Muundo wa (K/wi+mz)**

| Nambari | Majina | Vijenzi vyake | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | *Makongo* | Ma-kongo | Mitaro mingi na mikubwa iliyokatwa na maji ya mvua |
| 2. | *Matangi* | Ma-tangi | Matangi mengi |

Kutokana na mifano hii wakilishi, majina ya mahali katika kategoria hii yameundwa kwa mofimu mbili. Mofimu ya kwanza ni kiambishi cha wingi ambacho ni **ma-** katika nomino zote mbili na mizizi ambayo ni -**kongo** na -**tangi** mtawalia.

**Kielelezo***: Mpangilio wa Vipashio Kimsonge Katika Muundo wa (K/wi+mz)*

### 3.7 Muundo wa Kiwakilishi cha 'a' Unganifu na Mzizi (W/'a' ung+mz)

Baadhi ya majina ya mahali katika lugha ya Kikamba yenye muundo wa neno moja yameundwa kwa kiwakilishi cha 'a' unganifu inayotoa dhana ya umilikaji. Kiwakilishi hiki hubadilika kutegemea ngeli inayorejelewa. Ikiwa nomino inayorelelwa ni mlima ambao huitwa kiima (ngeli ya KYA -SYA) katika lugha ya Kikamba, kiwakilishi hicho huwa Kya-. Mifano kama: *Kyamutimba*, *Kyamunyaliti* na *Kyamuthei*. 'A' unganifu zikirejelea nomino zilizo katika ngeli tofauti zitawakilishwa kwa viwakilishi tofauti kama inavyodhihirika katika jedwali linalofuata.

**Jedwali: 3.7.1: Mifano wa Majina ya Mahali yenye Muundo wa (W/ 'a' ung+mz)**

| Nambari | Majina | Vijenzi Vyake | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1. | *Kyamuthei* | Kya-muthei | mlima wa mtu aliye uchi |
| 2. | *Kyamunyalit*i | Kya-munyaliti | mlima wa mtu anayegaragara |
| 4. | *Makaveti* | Ma-kaveti | Kitu kinachomilikiwa na mwanamke mdogo |

Mifano katika jedwali hili inaonesha kuwa baadhi ya majina ya mahali katika lugha ya Kikamba yameundwa kwa mofimu ya **'a'** unganifu na shina la neno. Mengi ya majina yaliyo na muundo huu yanataja majina ya milima ili kutofautisha milima yenyewe kwa sababu mingine huwa imekaribiana. Katika majina yenye muundo huu, kiwakilishi cha 'a'unganifu huunganishwa na mzizi wa neno ili kuunda jina moja tofauti na ilivyo katika lugha ya Kiswahili.

**Kielelezo 7: Mpangililio wa Vipashio Kimsonge Katika Muundo wa (W/ 'a' ung+mz)**

**5.0 HITIMISHO**

Makala hii imewasilisha uchanganuzi wa vijenzi vinavyounda majina ya mahali ya Kikamba na kanuni zinazotawala vijenzi hivyo zimefafanuliwa. Uchanganuzi umebaini kuwa majina ya mahali ya Kikamba yanayojibainisha kwa muundo wa neno moja moja yameundwa na vijenzi mbalimbali vinavyoweza kupangwa kidaraja au katika mchoro wa msonge. Makala hii imebaini kuwa majina ya mahali yenye muundo wa nomino moja yamejibainisha katiaka miundo saba tofauti ambayo ni: *muundo wa mzizi na kiambishi kielezi -ni cha mahali, muundo wa kiambishi cha ngeli, mzizi na kiambishi – ni cha mahali, muundo wa kiambishi kikanushi cha nafsi, mzizi, na kiishio (-a), muundo wa kiambishi cha udogo, mzizi na kiambishi -ni cha mahali, muundo wa kiambishi cha wingi na mzizi na muundo wa kiwakilishi cha 'a' unganifu na mzizi wa neno*. Yafaa ieleweke kwamba majina yote ya mahali katika jamii ya wakamba hayachukui maumbo yaliyojadiliwa katika makala hii tu. Kuna majina mengine ya mahali yaliyo na maumbo ya majina mawili ambapo jina la kwanza ni nomino na la pili ni kivumishi kama vile: *Mavia Meu* kwa maana ya mawe meupe, *Ndue Nguu* kwa maana ya mbega mzee n.k. lakini makali hii ilijikita tu katika majina yaliyoundwa kwa neno moja ili kubainisha vijenzi vyake.

**MAREJELEO**


Agard, F. (1984). *A Course in Romance Linguistics: A Synchronic view*. USA: Georgetown University Press.

Anido, C. (2016). "A Morpho-semantic Study of Toponyms: Lulogooli Place Names". University of Nairobi. PhD Thesis. Unpublished.

Buberwa, A. (2010). "Investigating Sociolingiustic Aspect of Place Names in Ruhaya in North-Western Tanzania". M.A.Dissertation (Unpublished). University of Dar es Salaam.

Cameron, K. (1961). *English Place Names*. Londan Batsford.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi. Phoenix.

Kadmon, N. (2000). Toponymy: *The Role, Laws and Languages of Geographical Names*. New York. Vantage Press.

Karama, M. (2021). "Ni Mvita Ni Mvita? Uchanganuzi wa Toponimu za Mitaa ya Mombasa, Kenya". *East African Journal of Swahili Studies*. Vol. 3(1). pp.78-90.

Kirui, R. (2013). "A Morpho-semantic Study of Kipsigis Toponyms". MA Thesis. Kemyatta University. Unpublished.

Lieber, R. (1990). *On The Organization of The Lexcon*. New York. Garland Publishing, Ink.

Massamba, D. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu, R. (1999). *Mtaala wa Isimu, Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi. Longhorn Publishers.

Mojapelo, M. (2009). "Morphology and Semantics of Proper Names in Northern Sotho". In *South African Journal of African Languages*. Vol. 2. Pp. 185-194.

Mphande, L. (2006). "Naming and Linguistic Africanism in African American Culture". In *Selected Proceedings of The 35$^{th}$ Annual Conference on African Linguistics*, ed. Mugane, J. pp.104-113. Somerville: MA: Cascadilla Proceedings Project.

Nida, E. (1949). *Morphology: A descriptive Analysis of Words*. Michigan. Michigan University Press.

Schotman, P. (2003). *Place Names and History in Dar es Salaam. Tanzania*. Netherlands: Leaden University Press.